

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA**

Barua zote ziandikwe kwa:

Simu	(Mkuu wa shule)	SHULE YA SEKONDARI IDUDA,
	(Makamu Mkuu wa shule)	S. L. P 33,
Unapojobu tafadhali taja:		MBEYA.
Kumb. Na.IDSS/Vol.1/1 S1551		Tarehe.....

---

MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI

.....  
S. L. P .....

**MBEYA.**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI IDUDA KIDATO CHA TANO JULY 2021/2021**

**HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA MKOA WA MBEYA**

1. Nafurahi kukujulisha kuwa mwanao.....amechaguliwa kwa tahasusi .....kujiunga katika shule hii kidato cha TANO 2021/2022. Tunampongeza kwa mafanikio hayo. Shule ipo umbali wa kilometra 16 toka makao makuu ya Mkoa.
2. Muhula wa masomo unaanza tarehe .....Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shulenii tarehe .....mwisho wa kuripoti ni tarehe .....
3. Mwanafunzi ambaye hatakuwa ameripoti shulenii ifikapo tarehe.....atahesabiwa kuwa ameikataa nafasi hii.
4. Tafadhali endapo hutajiunga na shule hii, kwa nafasi uliyopewa na Taifa, jibu kimaandishi kwa kutumia anwani ya shule hapo juu (Usijibu kwa njia ya simu)
5. Majibu yamfikie Mkuu wa shule kabla ya tarehe .....
6. Baada ya tarehe .....nafasi ya mwanao itajazwa na mtu mwengine kwa kufuata utaratibu wa uchaguzi uliowekwa na wizara.

**Yafuatayo ni maagizo ya kutimiza kabla ya kujiunga na shule hii**

- a. Jaza fomu ya kukubali kujiunga na shule hii iliyambatanishwa (tazama appendix D). Ijaze kikamilifu iwapo umekubali nafasi hii na iwapo utakubali kufuata mashariti / kanuni / taratibu / na sheria za shule hii kama KIAMBATANISHO “A” kinavyoonyesha.
- b. Nenda kwa Daktari wa Hospitali ya Serikali akapime na ajaze fomu ya “Medical Examination” iliyambatanishwa (tazama APPENDIX G)

- c. Jaza fomu ya ‘KUANDIKISHWA SHULENI NA HABARI ZA MWANAFUNZI / MZAZI / MLEZI ‘(Tazama APPENDIX D NA E)
  - d. Jaza fomu ya taarifa binafsi (Tazama Appendix H)
  - e. Jaza fomu ya uthibitisho wa uraia wa Mtanzania (Tazama Appendix F )
  - f. Fomu zote zilizotajwa hapo juu ufile nazo shuleni na kumkabidhi Makamu Mkuu wa Shule.
7. Pamoja na barua hii, naambatanisha sheria, kanuni na taratibu za shule. Wewe pamoja na Mzazi / Mlezi wako mnatakiwa kusoma kwa makini sheria, kanuni na taratibu zote zilizoainishwa na ikizingatiwa kuwa kigezo cha maendeleo ya kila mwanafunzi atakayejiunga na shule hii kitalenga katika maendeleo ya TAALUMA na NIDHAMU BORA pamoja na kazi za elimu ya kujitegemea.
8. HONGERA na KARIBU SANA IDUDA SEKONDARI.

**Saini ya Mkuu Wa Shule.....**

**Jina la Mkuu Wa Shule. SONGA, Y**

**Muhuri Wa Mkuu Wa Shule**

**Nakala :** Afisa Elimu Wa Mkoa,

S. L. P 256,

**MBEYA**

Afisa Elimu Jiji,

S. L. P 149,

**MBEYA.**

**1.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE****1.1 UTANGULIZI:**

Shule ya Sekondari IDUDA ilianzishwa mwaka 2005 iko Halmashauri ya Jiji la MBEYA na ipo kwa ajili ya kumjenga mwanafunzi wa Kitanzania kuwa mwenye tabia nzuri na mwenendo mzuri na hivyo kumwezesha kufanikisha lengo la maisha yake. Aidha, Sheria, Kanuni na Taratibu zinalenga pia katika kujenga amani, utulivu, umoja na furaha shulenii na kuwaandaa wanafunzi wote kuwa raia bora wa baadaye.

**1.2 Kauli Mbiu (MOTTO) ya Shule ni NIDHAMU TAALUMA NA MAZINGIRA** kwa hiyo tunategemea kuwa kila mwanafunzi atakayejiunga na shule hii atakuja kwa nia moja kuu ya kusoma kwa bidii na kuishi kwa Amani, Upendo na Ushirikiano katika jumuiya ya Shule hii ili hatimaye apate Elimu bora na aweze kulitumikia taifa letu hapo baadaye.

**1.3 Dira (Vision) katika shule ni “Elimu kwa mafanikio ya baadaye”**

**1.4** Aidha, katika utekelezaji wa dira ya shule ina dhamira (**mission**) yake isemayo, “**Kupambania Nidhamu na Elimu bora**”

**1.5** Kwa hiyo utasoma shule hii kwa kuzingatia maeneo hayo makuu matatu kauli mbiu, dira na dhamira ya shule hii kwa kufuata sheria kikamilifu, kanuni na taratibu zifuatazo ( na nyingine utakazopewa ) za shule:

**2.0 SEHEMU A: NIDHAMU KWA JUMLA ( TABIA NA MWENENDO)**

**2.1** Unatakiwa kuishi kwa amani, heshima na upendo. Sharti uwaheshimu Walimu na wafanyakazi wasio walimu walioko shulenii kama walezi wako pia uwaheshimu wanafunzi wenzako na viongozi wote wa Serikali ya wanafunzi. Hivyo basi ni marufuku kupigana, kutukanana, kutumia lugha chafu au kuanzisha / kushiriki vurugu za aina yoyote.

**2.2** Lazima uthamini na kutunza mali ya Umma. Hii ni pamoja na majengo ya shule ambayo ni nguvu za wananchi / walipa kodi. Endapo utafanya uharibifu, utahusika kufidia.

**2.3** Hautakiwi kutoroka shule, ukifanya hivyo basi utakuwa umejifukuza shule.

**2.4** Ukipatikana na kosa la wizi, ulevi, uasherati, kosa la kuolewa au kuoa, kubaka / kulawiti, kupata / kusababisha mimba au kutoa mimba, kudharau kuchana bendera ya taifa, UTAFUKUZWA SHULE MOJA KWA MOJA bila Msamaha.

**2.5** Shule sio uwanja wa malumbano ya kisiasa, wewe utajifunza URAIA na sio SIASA. Hivyo hairuhusiwi kutumia mazingira ya shule katika shughuli za kisiasa.

**2.6** Hairuhusiwi kuvuta Sigara / bangi, kuhifadhi na kutumia madawa ya kulevyo, kunywa pombe, kutembelea majumba ya starehe au nyumba za kufikia wagoni (guest houses)

**2.7** Ni lazima wakati wote kuonyesha nidhamu ya hali ya juu katika maongezi na walezi wako bila kutumia lugha chafu, kubishana, kukebehi, kuzomea, kuguna, au kuingiza mikono mfukoni wakati ukiongea na Mwalimu / mzazi / mlezi wako.

**2.8** Kugomea adhabu ni kosa kubwa liwezalo kukufukuzisha shule. Matatizo yote ni lazima yatatuliwe kwa kutumia taratibu halali zilizowekwa hapa shulenii kuanzia ngazi ya serikali ya wanafunzi, walimu wa madarasa n.k. Aidha ni marufuku kupeleka malalamiko yako moja kwa moja Mkuu wa shule au njie ya shule.

**2.9** Fujo, kelele, kuzomea, kukaa chini wakati Mwalimu au mkubwa ye yeyote aingiapo darasani, ni utovu wa nidhamu. Aidha hairuhusiwi kutoka darasani ovyo bila ruhusa ya Mwalimu au kiongozi wa darasa.

**3.0** Ni lazima usimame na kutoa salam pindi Mwalimu au mkubwa ye yeyote anapopita karibu yako

**3.1** Unatakiwa kuheshimu kengele za shule, hii ni pamoja na kuwahi sehemu yoyote unayotakiwa bila kuchelewa. Ukichelewa hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yako.

**3.2** Ni marufuku kutembea au kuingia katika nyumba za walimu au wafanyakazi bila ruhusa maalum.

**3.3** Lazima uheshimu tarehe ya kufungua shule. Unatakiwa kuripoti shulen na kuanza masomo kwa kuzingatia tarehe rasmi iliyopangwa.

**3.4** Utasimamishwa shule wiki tatu endapo utabainika kudanganya mitihani ya ndani.

#### **4.0 SEHEMU B: MAKOSA YAWEZAYO KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE MOJA KWA MOJA BILA MSAMAHA:**

- i. Wizi
- ii. Kutohudhuria masomo zaidi ya siku 90 bila taarifa / utoro
- iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo
- iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu / walezi na jamii kwa ujumla.
- v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga Mwalimu au na mtu ye yote Yule.
- vi. Kukata nywele kwa mtindo usiokubalika na uongozi wa shule (Viduku haviruhusiwi).
- vii. Kufuga ndevu.
- viii. Ulevi / unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevy.
- ix. Uvutaji wa Sigara
- x. Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.
- xi. Kusababisha ujauzito (wavulana), kupata ujauzito (wasichana) na kutoa mimba.
- xii. Kupata ujauzito au kutoa mimba
- xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
- xiv. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana
- xv. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
- xvi. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
- xvii. Kudharau bendera ya taifa.
- xviii. Kufanya jaribio lolote la kujiu, au kutishia kujiu kama kunywa sumu n.k.
- xix. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

#### **5.0 MAHITAJI YA LAZIMA SHULENI**

##### **6.1 SARE YA SHULE**

###### **A. WAVULANA**

- i. Suruali mbili za rangi nyeusi na rangi ya **kijivu iliyokolea** za heshima siyo modo.
- ii. Mashati mawili yenyeye mikono mirefu aina ya tetron. Mashati yote ni lazima yawe marefu yavezayo kuchomekewa ndani ya suruali, mfuko mmoja usio na mfuniko uje nayo.
- iii. Jozi (pair) mbili za viatu vyeusi vya ngozi vya kamba. Visiwe na visigino virefu “ghorofa” au soli nene kupita kiasi. Viwe viatu vya kawaida vya heshima visiwe vya ajabu. Aidha huruhusiwi kuva raba au buti.
- iv. Soksi za rangi nyeusi uje nazo
- v. Masweta mawili ya rangi ya **Brauni** na **Blue** iliyokolea yenyeye “**V- SHAPE**” sehemu ya shingo uje nayo
- vi. Raba nyeupe jozi moja na nguo za michezo (**Track suit ya rangi ya kijivu iliyokolea** yenyeye **michirizi mieupe pembeni**)
- vii. Tai mbili za rangi **nyeusi** na **Kijivu iliyokolea**

###### **B. WASICHANA**

- i. Mashati mawili meupe aina ya tetron mikono mirefu yawe marefu kuweza kuchomekea
- ii. Jozi mbili za viatu vyeusi vya ngozi vya kamba visivyo na visigino virefu au “ghorofa” au soli nene kupita kiasi pia zisiwe raba.
- iii. Soksi ndefu nyeupe jozi mbili au zaidi.
- iv. Masweta mawili ya rangi ya Brauni na Blue iliyokolea yenyeye “**V-SHAPE**” sehemu ya shingo uje nayo.
- v. Sketi mbili za rangi nyeusi na rangi ya **kijivu iliyokolea** zenye urefu wa kutosha nchi mbili kutoka kwenye viatu (**Sketi zishonwe kwa Mtindo wa Rinda box**)
- vi. Tai mbili za rangi **nyeusi** na **Kijivu iliyokolea**
- vii. Raba nyeupe jozi moja na nguo za michezo (**Track suit ya rangi ya kijivu iliyokolea** yenyeye **michirizi mieupe pembeni / ubavuni**)

**NB: Uniform nyeusi itavaliwa siku ya Jumatatu na Jumanne, Rangi ya Kijivu iliyokolea itavaliwa siku ya Jumatano na Alhamis NA Track Suit itavaliwa siku ya Ijumaa kwa ajili ya michezo.**

NAPENDA KUTAHADHARISHA KUWA MZAZI / MLEZI YEYOTE AMBAYE ATAMNUNULIA  
MTOTO WAKE SARE ISIYOTAKIWA ATALAZIMIKA KUNUNUA NYINGINE KADRI YA  
MAELEKEZO.

## **KIAMBATANISHO C**

### **KARO YA SHULE**

Karo ya shule ni Tsh. Elfu ishirini tu 20,000 kwa mwanafunzi wa kutwa. Unaweza kulipa kiasi cha shilingi 10,000 kwa mwanafunzi wa kutwa kwa muhula au kulipa ada yote kwa mara moja pamoja na michango yote ilioainishwa hapo chini. Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule **A/C NO. 6106600175 NMB** Jina la Akaunti **SCHOOL FUND IDUDA SECONDARY**

#### MICHANGO MINGINE:

1. TAALUMA TSH.....20,000/=
2. TAHADHARI.....5,000/= (Haitarejeshwa)
3. ULINZI NA VIBARUA.....30,000
4. KITAMBULISHO TSH.....6,000/=
5. STAMP SIZE.....(PICHA 02)
6. UKARABATI WA SAMANI.....15,000/=
7. NEMBO YA SHULE.....2,000/=
8. MITIHANI YA KUJIPIMA (MOCK ).....20,000/=
9. HUDUMA YA KWANZA.....10,000/=
10. BIMA YA AFYA.....5,000/= (*Lazima mwanafunzi aje na kadi ya Bima ya Afya ambayo yeye ameilipia NHF kikaya*)
11. MALIPO YOTE YA MITIHANI KAMA VILE JOINT, MOCK NA NECTA YATALIPWA KWENYE AKAUNTI NA UTAJULISHWA WAKATI HUO

#### MICHANGO YOTE HULIPWA KWA MKUPUO

NB: Malipo utakayolipia Bank ya NMB Tafadhali uje na RISITI (Bank pay in slip) zote kwa mhasibu wa shule.

### **MAHITAJI MENGINE**

1. Counter Books (Quire 4) zisizopungua nane (08) kwa ajili ya notes za masomo darasani
2. Faili moja kwa ajili ya kuhifadhi nyaraka za mwanafunzi
3. Rimu moja ya karatasi za photocopy (A4 SIZE)
4. Fagio mbili za nje na ndani
5. Ndoo mbili zenyenye mifuniko
6. Mwanafunzi aje na jembe na hard broom kwa ajili ya chooni
7. Mkebe wa vifaa vya Hisabati (mathematical set) kwa wale wenye Hisabati
8. Vitabu vya ziada kwa ajili ya kujisomea kulingana na Mchepuo wake, naambatanisha orodha ya vitabu anavyotakiwa awe navyo.
9. Aje na kamusi ya masomo yake kwa wanafunzi wanaosoma kiingireza waje na kamusi ya Oxford – Advanced Dictionary.
10. Begi ya kuwekea vitabu
11. Kila mwanafunzi atakayesoma somo la Elimu ya viumbe (Biology) aje na “Dissecting kit” seti pamoja na **Tray yake**
12. Scientific calculator kwa wanafunzi wanaosoma masomo ya Sayansi.
13. Kwanja 1, Jembe 1, Reki 1, Mifagio ya ndani na nje.
14. MUHIMU: MWANAFUNZI AJE NA NAKALA YA HATI YA MATOKEO (RESULT SLIP) YA KIDATO CHA NNE.

## **ORODHA YA VITABU MUHIMU KWA KILA SOMO**

Unashauriwa kumnunulia mwanao vitabu kulingana na masomo anayosoma. Orodha ya vitabu vinavyotakiwa kwa kila idara ni kama ifuatavyo:-

<b>GENERAL STUDIES</b> <ol style="list-style-type: none"><li>1. General studies for Advanced level certificate, form six (6) by Richard R.F Mbalase(2011)</li><li>2. General Studies for Advanced level certificate, form five (5) by Richard R. F Mbalase (2011)</li><li>3. Contemporary approach for Advanced level (General Studies Notes" Form five (5) and Form six (6) by Nyambari C. M Nyangwine, Steven O. Maluka (New syllabus 2009)</li></ol>	<b>ENGLISH</b> <ol style="list-style-type: none"><li>1. Macmillan Education Ltd 2000, Encounters from Africa, Macmillan</li><li>2. Ayi Kwei Amah, 1996, The Beautiful Ones Are Not Yet Born, EAEP</li><li>3. Chinua Achebe, 1991, A Man Of The People, BAEP</li><li>4. Ndunguru 1999, Divine Providence, Mkuki Na Nyota.</li><li>5. Magala Nyago, 1985, The Rape of The Pearl.</li><li>6. Namige Kayondo, 1985 Vanishing Shadows, Macmillan.</li><li>7. Danny Sato, 1983, His Excellency the Head of State, Macmillan.</li><li>8. David Ommowale, 2002, A Season Of Walting, EAEP</li><li>9. Francis Lubuga, 1990, Betray In The City, Heinemann</li><li>10. Ngugi Wa Thiong'o, et all 1982, I Will Marry When I Want, EAEP</li><li>11. Bukenya, 1984, The Bride, EAEP</li><li>12. Okot Omotah 1991, Lwanda Megere Heinemann</li><li>13. Henrick Ibsen, 1974, An Enemy Of The People, Eyre Matheuen</li><li>14. John Ruganda 2005, Black Mamba, EAEP</li><li>15. Charles Mloka, 2002, The Wonderful Surgeon And Other Poems, Mkuki Na Nyota.</li><li>16. Tanzania Institute of Education, 1996, Selected Poems, Print Pak (T) Limited.</li><li>17. The Real English Textbook Advanced Level, Dr. Kadeghe Michael.</li></ol>
<b>HISTORY</b> <ol style="list-style-type: none"><li>1. Major issues in African History in Tanzania Institute of Education</li><li>2. History of Modern Europe by Peacock</li><li>3. How Europe Underdeveloped Africa by W. Rodney</li><li>4. History in Focus: Modern World History by Ben Walsh</li><li>5. Mastering Advanced level History book Two, by Kato, A (2011)</li><li>6. Mastering Advanced level History Book One by Kato, A (2021)</li></ol>	
<b>GEOGRAPHY</b> <ol style="list-style-type: none"><li>1. Principle of Physical Geography by Monkhouse (2008)</li><li>2. Landforms in Africa by Collin Buckle</li><li>3. Statistics Simplified by N. A Saleem</li><li>4. Map Reading by Mac Master</li><li>5. Human and Economics Geography by C. Morgan (1982)</li><li>6. Map Reading, General Publications Ltd – DSM by Durra, S. E. (2003)</li><li>7. Geography an Integrated Approach: Fouth edition by David Waugh (2009)</li><li>8. Practical Geography for Africa by John M. Pritchard (1990)</li><li>9. R. B. Bunnet (2007) General Geography in Diagrams</li></ol>	

## **PHYSICS**

1. Advanced Level Physics 6<sup>th</sup> Edition by Nelkon And Parker (1989)
2. Advanced Physics by Tom Duncan
3. Advanced Physics Paper 1 and Paper 2 by E. Njau (2002)
4. Principle of Physics for Class XI & XII by S. Chand (2011)
5. A-Level Physics Fourth Edition by Roger Muncaster (Fourth Edition) 1993

## **MATHEMATICS**

1. Scientific Calculators
2. Basic and Applied Mathematics by Respicius Kiiza (2010)
3. Mathematics by for Class XI & XII by DASS, H.K & VERMS, R. (2000)
4. Pure Mathematics (Revised Ed) by M. F. Macrae (2011)
5. Pure Mathematics For Advanced Level Volume 1& 2 by Backhouse, K.K (1985)
6. Core Mathematics For Advanced Level by L. Bostock
7. Advanced Level Mathematics by L. K Shayo
8. Advanced Level Mathematics Vol. & II by Kinunda (1974)

## **BIOLOGY**

1. Dissecting Kit
2. New Understanding Biology For A – Level Student by Glenn & S. Toole (1999)
3. Systematic and Classification by L. K Msaki (1993)
4. Biology, A functional Approach by M. B. V. Roberts (1971)
5. Advanced Biology: Principle and Application by C. J. Clegg & D. G. Mackean (2000)
6. Biological Science by Taylor, et all (1997)
7. S. Chand's Biology for Class XI & XII by P.S Verma & B. P Pandey (2005)
8. Guide to Dissection by H. G. Q Rowett (2005)

## **CHEMISTRY**

1. Advanced Chemistry Physical and Industrial by P. Mathew (2006)
2. Essential of Physical Chemistry by Arun Bahil, B. S Bahil & G. D Tuli (2012)
3. Organic Part A & B by A. Abdullah & M. H. Nkunya.
4. Inorganic Part A & B by J.S Moro Guterman & M. Mikesewala (1989)
5. Physical Chemistry by Dungu & J.B.A Mihigo (1998)
6. Advanced Level Inorganic Chemistry Part I & Part II by Tanzania Institute of Education (1995)
7. Organic chemistry and introduction by Jack E. Fernandez (1982)
8. Understanding Chemistry for A Level Student
9. Conceptual Chemistry for Class XI & XII by S. K Jaini (2011)
10. Advanced Level Chemistry, Fouth Edition by E. N Ramsden (2000)

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA**  
**SHULE YA SEKONDARI IDUDA**

**FOMU NAMBA 10, 11, 12, 13 NA 14 ZIRUDISHWE SHULENI WANAPORIPOTI**

**FOMU YA KUKUBALI**

1. Mimi.....msichana / mvulana, ninakubali kuingia kidato cha .....  
..... shule ya Sekondari Iduda kama mwanafunzi wa kutwa tarehe .....  
nitafika shulenii bila kuchelewa.
2. Nitatii sheria za shule na nitaishi kwa amani. Nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kazi za kujitegemea
3. Sitashiriki katika Migomo, Fujo na makosa ya jinai.
4. Saini ya Mwanafunzi.....Tarehe.....

**SEHEMU YA MZAZI / MLEZI**

1. Mimi .....ninakubali mtoto wangu.....  
Asome katika shule ya sekondari Iduda kuanzia tarehe .....
2. Ninaahidi kulipa Ada na Michango na pia kumpatia vitu vyote anavyotakiwa kuwa navyo shulenii kama ilivyotajwa katika Barua na Fomu ya kujiunga na shule.
3. Ninakuhakikishia kwamba nitamwonya mtoto wangu kutii sheria za shule na kuishi maisha mazuri na kuwa na bidii kwenye masomo na kazi za kujitegemea
4. Ninakubali kuwa mtoto wangu amekubaliwa kuingia katika shule ya sekondari Iduda kama mwanafunzi wa kutwa.
5. Anuani yangu ya kudumu ni.....Simu no.....
6. Saini .....Tarehe .....

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA**

**SHULE YA SEKONDARI IDUDA**

**FOMU YA KUMWANDIKISHA MWANAFUNZI SHULENI**

(Jaza Formu Hii Kwa Umakini)

1. Jina kamili la Mwanafunzi .....
2. Tarehe ya kuzaliwa .....
3. Kabilia ..... Uraia ..... Dini .....
4. Jina la Mzazi .....
5. Anuani ya Mzazi ..... Kazi ya Mzazi ..... Simu Na.....

**SEHEMU HII IJAZWE NA WANAFUNZI AMBAO HAWAKAI NA WAZAZI WAO**

6. a) Jina la Mlezi .....
- b) Uhusiano kati ya Mlezi na Mwanafunzi.....
- c) Kazi ya Mlezi ..... Simu Na.....
- d) Anuani ya Mlezi .....
7. Shule atokayo Mwanafunzi .....
8. Wakati wa Likizo mwanafunzi atakwenda wapi ? .....
9. Maelezo ya Mwanafunzi .....
10. Ujuzi (stadi) mwingine .....
11. Saini ya Mwanafunzi ..... Tarehe .....

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA**

**SHULE YA SEKONDARI IDUDA**

**MKO A WA .....**

**Ofisi Ya Mkuu Wa WilayaYa .....**

**S. L. P .....**

**MBEYA.**

**Tarehe.....**

**Mkuu Wa Shule,**

.....  
.....  
.....

**UTHIBITISHO WA URAIA WA TANZANIA**

Nathibitisha kuwa ..... (Jina kamili la Mwanafunzi) ni raia wa Tanzania kwa kuzaliwa / kwa kuandikishwa.

Baba yake (Jina kamili) .....

Amezaliwa katika Mko wa ..... Wilaya ya .....

Tarafa ya ..... Kata ya .....

Majina yake (Jina Kamili) .....

Amezaliwa katika kata ya ..... Wilaya ya .....

.....

**MKUU WA WILAYA**

**NB:** Kila mwanafunzi analazimika kuishughulikia hati hii kikamilifu. Ikishajazwa irudishwe kwa Mkuu wa shule siku ya kuripoti shuleni. Au leta nakala ya Cheti cha Kuzaliwa badala ya fomu hii.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA**  
**SHULE YA SEKONDARI IDUDA**

IDUDA SECONDARY SCHOOL,  
P.O BOX 33,  
MBYEYA

.....  
TO MEDICAL OFFICER.....  
.....  
.....

**PART A**

Mr. / Miss .....

Please examine the above named student as to his / her physical and mental fitness for a full time student in this school. The examination should include the following categories

1. Haemoglobin .....
2. P. V. Bleeding .....
3. Sight .....
4. Blood pressure .....
5. Urine for Sugar .....
6. Stool for routine examination .....
7. Pregnancy test .....
8. Skin diseases .....
9. Leprosy .....
10. Any deformity .....
11. Epilepsy .....
12. Pulmonary tuberculosis .....
13. Neurosis .....
14. Venereal diseases.....
15. Other diseases .....

**PART B**

**MEDICAL CERTIFICATE**

**(To be completed by a Government Medical Officer)**

1. I have examined the above named student and consider that he / she is physically fit / unfit and mentally fit / unfit for a full time schooling.
  2. Other comments:.....
  3. Date .....Signature .....
- Station .....Designation.....